2nd Floor New Safari Hotel, Arusha Tanzania

P.O.BOX   ARUSHA, TANZANIA

Phone: +255 759 652 103

Email:   info@jmmfoundation.org

Website:   https://JmmHeartFoundation.org

**Josephine Mohamed Memorial Heart Foundation (JM Memorial Heart Foundation)** Ni asasi ya kiraia yenye usajili wa kisheria Namba **OONGO /R/ 3569** na inafanya kazi zake nchini Tanzania.

Lengo kuu la taasisi hii ni kusaidiana na Serikali katika kutatua changamoto za magonjwa ya moyo na matatizo yanayotokana na magonjwa ya moyo. Ili kufikia lengo hili kuu, JM Memorial Heart Foundation ina malengo mahususi ambayo ni pamoja na:-

1. Kutoa elimu na kuhamasisha watu kujua hali ya afya zao mara kwa mara hususani mambo yanayohusiana na moyo (Create awareness and make sensitization). Hii ni pamoja na kuhamasisha upimaji wa hiari ili watu wajue hali ya afya zao na kuchukua hatua stahiki.

2. Kuunganisha nguvu ya pamoja katika mapambano dhidi ya magonjwa na matatizo yanayohusiana na moyo (Community participation). Hii inasaidia kuboresha afya ya jamii na hata mgonjwa kupona kabisa, badala ya mgonjwa kubeba tatizo lake mwenyewe, jamii inalibeba kwa pamoja kupitia JM Memorial heart foundation

3. Kumsaidia mgonjwa kupata huduma na vipimo katika hali rahisi na ya wepesi. Wakati mwingine wale wenye maisha duni walioko pembezoni wanapata msongo wa mawazo( stress) kutokana na mazingira magumu wanayokutana nayo wakati wa kutafuta tiba. JM Memorial heart foundation inawaelekeza namna bora na sehemu sahihi ya kupata tiba ya matatizo ya moyo.

4. Kupata wataalamu na vifaa tiba kwa ajili ya kupambana na matatizo ya moyo. Katika kuunganisha nguvu ya pamoja kupitia michango ya wahisani na wadau mbalimbali, kwa kushirikiana na taasisi binafsi na serikali ikiwa ni pamoja na wizara ya afya, taasisi itaweza kuandaa wataalamu wa tiba na kupata vifaa tiba. Hivyo jamii itaweza kupata huduma kwa gharama nafuu zaidi, kwa karibu na kwa haraka zaidi. Kwa namna hii tunaweza kuokoa maisha ya watu wengi zaidi.

**Dira/mission**: Kuelimisha umma kuhusu ugonjwa wa moyo, kuchochea utambuaji wa viashiria vya awali, na kusaidia utafiti kuhusu matatizo ya ugonjwa wa moyo (to educate the public about heart disease, promote early detection and support pioneering research)

**Maono/Vision**: Kuelimisha na kusaidia watu ambao hawana taarifa muhimu na uwezo wa kupata matibabu stahiki ya ugonjwa wa moyo(to educate and help people who lack access to crucial information and resources to fight heart related challenges)

Mahitaji ya taasisi

Ili kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu taasisi inahitaji rasilimali watu, fedha na vifaa kama ilivyoainishwa hapa chini:

a)Rasilimali watu: wataalamu wa magonjwa ya moyo(Cardiologists), wauguzi(Nurses), wataalamu wa maabara(lab technicians) na watendaji wa taasisi kama watehama na wengine.

b)Vifaa kama machine za kupima uzito na kimo, Body Mass Index Charts, pulse oxmeter, ECG machine, ECHO/Vscan machine, RGB, Cardiac Enzyme, valvu na betri za moyo, Computer, Printers, ambulances na mobile clinic vehicle.

## JM Memorial Heart Foundation imeshafanya nini hadi sasa?

- JM Memorial Heart Foundation imeshatembelea mashirika kadhaa, taasisi binafsi, za dini, na za serikali zilizopo Arusha mjini na Karatu, na kutoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari wa afya ya moyo.
- Taasisi ilishafanya kambi za matibabu( Medical camp) katika eneo la Karatu mjini ambapo watu takribani 500 walijitokeza kujiandikisha na tulifanikiwa kuwahudumia watu 200 tu kwa sababu ya ufinyu wa bajeti iliyokuwepo.

## Taasisi ina nini mpaka sasa?

- JM Memorial Heart Foundation ina bodi inayosimamia na kuratibu shughuli na miradi inayoendeshwa na taasisi, na baadhi ya wataalumu ambao wanafanya kazi kwa moyo wa kujitolea ili kufikia maono ya taasisi.
- JM Memorial heart foundation inayo ofisi(Physical contact) Arusha mjini inayotumika kuratibu shughuli na miradi yake .
- Taasisi pia inajivunia uwepo wa amani katika nchi ya Tanzania na Serikali sikivu inayojali afya za wananchi na hivyo kuwa na mazingira wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kila siku.
- Portal ya kubaini watu wenye changamoto za moyo

Matarajio ya Taasisi.

- Taasisi inatarajia kufanya kambi za vipimo na matibabu ili kugundua viashiria mbalimbali vya awali vya magonjwa ya moyo ( Medical camping and detection of early indicators of heart complications and diseases). Ili kufanikisha hili, taasisi ina portal maalum ambayo itatusaidia kupata taarifa ya hali ya afya ya moyo katika maeneo mbalimbali.
- Taasisi inatazamia kuendesha clinic za kuhamahama( mobile clinic). Mradi huu unatakiwa kuwa na gari maalumu ambalo shughuli zote za matibabu zitafanyika humo ili kuepuka kukodisha mahema na gharama nyingine.
- Taasisi inatazamia kununua vifaa tiba kama vile valvu na betri za moyo n.k, pamoja na kuwa na maduka ya madawa kwa ajili ya matibabu ya moyo yaani famasi, ktk maeneo yaliyo mbali na famasi zilizopo za madawa ya magojwa ya moyo.

Ombi la taasisi kwa Serikali kupitia wizara ya afya

Mh. waziri,Taasisi ina lengo la kufanya kazi kwa karibu na Serikali lakini changamoto inayotukabili ni ufinnyu wa bajeti ya utekelezaji wa miradi tajwa.

. Mh.waziri, bajeti yetu kwa mwaka inayotokana na makusanyo ya ndani (local contribution) ni Tsh milioni mia sita na hamsini ( 650,000,000), na mpaka sasa tumefanikiwa kukusanya Tsh milioni mia na hamsini (150,000,000) kutoka kwa wahisani mbalimbali na watu wenye mapenzi mema. Hivyo tumepungukiwa na kiasi cha Tsh milioni mia tano (500,000,000) ili kukamilisha malengo yake ya mwaka

.Mh. waziri tunaomba wizara unayoiongoza ituwezeshe kupata uwezo ili miradi na mipango ya taasisi yetu itekelezwe kwa wepesi na ufanisi.

Mh. waziri, tumeandaa portal yenye lengo la kubaini changamoto za awali za magojwa ya moyo inayoitwa **jmmhf portal.** Tunakuomba ikikupendeza itumike kwenye hospitali zetu kwa lengo hilo la kubaini viashiria vya awali vya magonjwa ya moyo.

Kwako binafsi mh. waziri, kwa kuwa wewe unafahamiana na taasisi  nyingi ndani na nje  ya nchi,tunakuomba utuunganishe na wadau, wahisani na wafadhili mbalimbali watakaoweza kuisaidia taasisi yetu.

ASANTE KWA MUDA WAKO